

**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA KAGERA MHESHIMIWA  
MEJA JENERALI (MST) SALUM M. KIJUU WAKATI WA  
UZINDUZI WA DUKA LA DAWA KATIKA HOSPITALI YA  
RUFEE YA MKOA WA KAGERA, TAREHE 17 AGOSTI, 2017**

**Ndugu Katibu Tawala wa Mkoa,  
Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,  
Mstahiki Meya wa Manispaa ya Bukoba,  
Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri,  
Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri,  
Ndugu Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Hospitali,  
Watumishi wa Hospitali,  
Waandishi wa Habari  
Waalikwa wote,  
Mabibi na Mabwana.**

**Kagera! Kazi, Amani na Maendeleo.  
Kazi, Amani na Maendeleo! Kagera.**

**Ndugu Wananchi,**

Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha salama katika ufunguzi huu wa Duka la Dawa la Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wetu.

Natambua umuhimu wa huduma hii hasa katika maendeleo ya jamii. Kwani tukiwekeza katika huduma za afya tutakuwa na taifa lenye nguvu kiuchumi na maendeleo kwa ujumla.

## **Ndugu Wananchi,**

Kwa kipindi kirefu kumekuwepo na upungufu mkubwa wa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya ikiwemo Hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa. Kwa kipindi cha nyuma Hospitali hii ilikuwa ni kati ya Hospitali zenye wagonjwa wengi wanaokwenda nje kununua dawa baada ya dawa hizo kukosekana ndani ya Hospitali.

Kufuatia hali hiyo, na kwa kutekeleza agizo la Serikali, iliamriwa lifunguliwe Duka la Hospitali. Duka hili ni maalum kwa ajili ya kuuza dawa hasa zile ambazo zinahitajika lakini hazipatikani katika Bohari ya Dawa (Medical Stores Department - MSD). Lengo letu ni kuhakikisha dawa za msingi zinapatikana ndani ya Hospitali na hivyo kumpunguzia mgonjwa usumbufu wa kwenda nje kununua dawa tena kwa bei ya juu.

Nimpongeze Katibu Tawala wa Mkoa, Mganga Mkuu wa Mkoa na timu nzima ya uongozi wa Hospitali, Bodi ya Hospitali iliyomaliza muda wake kwa kusimamia na kuhakikisha Duka hili linakuwepo na linaanza kutoa huduma.

Nimetaarifiwa kuwa uanzishwaji wa duka hili umetumia mkopo wa fedha; yaani takribani shilingi milioni ishirini na mbili ( TSH 22M) zimetumika kukamilisha matengezo miundombinu ya duka na kiasi cha shilingi milioni thelathini (TSH 30M) zimetumika kwa ajili ya manunuzi ya dawa za kuanzia. Hongera sana.

## **Ndugu Wananchi,**

Duka hili ni lenu. Litumieni ili liwasaidie. Tutaendelea kuwa na dirisha la siku zote la dawa zinazopatikana na kutolewa kwa mfumo wa kawaida. Dawa zitakazokosekana kwenye dirisha hilo la kawaida sasa mtazipata kwenye duka hili badala ya kusumbuka kwenda nje ya Hospitali tena wakati mwingine usiku. Lakini tukumbuke katika duka hili dawa zote zinauzwa kwa bei

nafuu, hivyo lazima mteja awe na fedha au kadi ya Bima ya Afya. Ni muhimu hili likawekwa wazi ili lisije likaleti malalamiko hasa kwa makundi ya msamaha.

Wataalamu wamenieleza kuwa bei za dawa katika duka hili ziko chini ukilinganisha na maduka ya nje. Kimsingi bei lazima ziwe chini kwa sababu hatulipi kodi ya pango, tunatumia majengo ya Serikali, baadhi ya watumishi wanaofanyakazi katika duka hili wanalipwa mshahara na Serikali kwa kodi zenu wananchi, hivyo duka hili litaendelea kuuza dawa kwa bei za chini ukilinganisha na maduka ya nje.

### **Ndugu Wananchi,**

Duka hili lilianza kufanyakazi tangu tarehe 01 Agosti, 2017 kama sehemu ya maandalizi na majaribio. Nimefarijika kusikia kuwa kwa kipindi hicho, idadi ya wagonjwa wanufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwenda nje ya Hospitali hii kupata dawa imepungua. Lengo letu ni kuhakikisha kuwa hakuna mgonjwa anayekwenda nje ya Hospitali kununua dawa, wote wapate dawa ndani ya uzio wa Hospitali.

### **Ndugu Wananchi,**

Nitoe wito kwa viongozi wa Hospitali kuhakikisha kuwa duka hili linaendelea kuwepo na kuboreshwa ili litoe huduma nzuri zaidi. Nina imani kuwa uongozi wa Hospitali, chini ya usimamizi wa Bodi ya Ushauri ya Hospitali ambayo pia nimeizindua leo, mtashirikiana kuhakikisha duka linazidi kutoa huduma nzuri siku hadi siku. Hakikisha dawa zote za msingi zinapatikana na duka linatoa huduma masaa 24 kila siku.

Ninatambua changamoto zilizopo hasa upungufu wa watumishi. Lakini jipangeni ili kwa watumishi waliopo duka hili lifanye vizuri.

Watumishi wasimamiwe wafanye kazi kwa uadilifu na uaminifu, wasifanye kazi kwa maslahi binafsi, wawe na lugha nzuri ya kuwavutia wateja. Mapato na matumizi ya duka ili yawekwe wazi kwa uongozi unaosimamia na watumishi wote wa Hospitali hii.

Lengo letu liwe ni kupanua duka hili ili litoe huduma kwa Zahanati na vituo vya afya katika Mkoa mzima. Yaani badala ya vituo hivyo kwenda kununua dawa, zinazokosekana MSD, kwa maduka binafsi waje wanunue dawa hizo hapa.

### **Ndugu Wananchi,**

Mwisho, napenda kuwashukuru wote ambao mmeshirikiana nasi leo. Ninaomba tunapotoka hapa wote tuwe mabalozi wa kuwaelimisha wananchi juu ya uwepo wa duka hili ili waje kupata huduma.

Baada ya kusema hayo, sasa ninatamka kuwa Duka la Dawa la Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera sasa limezinduliwa rasmi.

**Kagera!** Kazi, Amani na Maendeleo.

**Kazi, Amani na Maendeleo!** Kagera.

***“ASANTENI KWA KUNISIKILIZA”***